**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO

**ZABUNI NA: LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT...**
**TAREHE: 20/05/2021**

# TANGAZO LA ZABUNI YA KUTOA HUDUMA MBALIMBALI KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

1. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inakusudia kubinafsisha huduma mbalimbali kwa mwaka wa Fedha **2021/2022.**

2. Zabuni hii itaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 (2011) na Kanuni zake za mwaka 2013, Tangazo la Serikali Na. 446 na marekebisho yake ya mwaka 2016.

3. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inawakaribisha Makampuni, Vikundi au watu binafsi wenye nia na uwezo wa kufanya kazi zifuatazo:

| NAMBA YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI |
|---|---|
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT01** | Zabuni ya kujenga choo cha Umma katika Stendi ya Masika kwa mfumo wa kujenga, kuendesha na kurejesha. |
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT02** | Zabuni ya kujenga choo cha Umma katika bustani ya sabasaba kwa mfumo wa kujenga, kuendesha na kurejesha. |
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT03** | Zabuni ya kukusanya ushuru wa maegesho ya magari katika maeneo mbalimbali yanayomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro |
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT04** | Zabuni ya kukusanya ushuru wa vyoo mbalimbali vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro |
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT05** | Zabuni ya kukusanya ushuru wa masoko mbalimbali yanayomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro |
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT06** | Zabuni ya kukusanya ushuru wa mchanga katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro |
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT07** | Zabuni ya kufanya usafi wa barabara na mifereji ya maji ya mvua katika barabara zenye jumla ya urefu wa KM 51.9 katika Manispaa ya Morogoro |

| | |
|---|---|
| **LGA/079/2020-21/HQ/NCS/17 LOT08** | Zabuni ya kutoa huduma ya utunzaji wa bustani pamoja na mizunguko ya barabara mbalimbali katika Manispaa ya Morogoro |

4. Nyaraka za Zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya Tshs. 50,000/= (Ada hiyo haitarejeshwa) na utaratibu wa malipo unapatikana ofisi kuu.

5. Ombi la zabuni liwe na jina na anuwani ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi yake ilipo kwa sasa.

6. **ZINGATIA**: fomu ya maombi ya zabuni ijazwe na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney) katika zabuni hii.

7. Mwombaji atatakiwa aambatanishe nyaraka mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha zabuni.

8. Mwombaji aambatanishe kivuli cha stakabadhi ya ada ya maombi wakati wa kurejesha zabuni.

9. Waombaji wanaweza kukagua nyaraka za zabuni na kupata maelezo kutoka kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro S.L.P. 166 Morogoro siku ya Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za Sikukuu za Kitaifa.

10. Mwombaji wa zabuni anahitajika kuleta kiapo cha dhamana (bid securing declaration) kama kilivyoainishwa kwenye kitabu cha zabuni

11. Masharti na vigezo vingine vinapatikana katika kitabu cha zabuni.

12. Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) moja na nakala kivuli mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Zabuni **Na. LGA/079/2021-21/HQ/NCS/17LOT.. ya (ingiza maelezo ya zabuni unayoomba)** Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa anuani ifuatayo:- **Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, S.L.P 166, Morogoro**.

13. Siku ya mwisho ya kuwasilisha zabuni ni **tarehe 02 Juni, 2021 saa (6.00) sita kamili adhuhuri**. Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu, mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni hizo katika ukumbi wa Manispaa.

14. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielektroniki, na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji Zabuni, kwa hali yoyote ile Zabuni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

*Sheilla E. Lukuba*
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**MOROGORO**